## Kwako bibi

# Kumbe bwana maskini aweza kufukuzwa na mkewe ?

Tangu wakati wa mababu zetu na kufuatana na maadibisho ya makanisa, mme ndiye mwenyi kuhitajiwa kuwa mkubwa wa jamaa. Hata serkali nayo yaamini jambo hilo.

Watu wengi wamesikia vibaya mbinu hiyo kwa ginsi wapenda kumtesa bibi na kumgeuza sawa mtumwa. Hawampatie feza za posho kama vile inavyotakika. Na wengine wamupiga makofi na vipasi na hata kumfukuza nje ya nyumba usiku. Mifano ni mingi na yaonekana hapa na kule. Watu wamoja wamoja wapo hakika kuwa jambo kama hilo ni la kawaida.

Akina dada wengi hukataa kabisa kushika ao kuona tabia hiyo na kufanya nguvu ili wajitoshe katika utumwa wa namna hiyo. Pahali pa kusikilizana nyumbani akina dada wamoja wamoja waanza kuwaonyesha mabwana zao cha mutema kuni. Kwa kutafuta "uhuru" wao, hutenda mambo mbali mbali sawa vile :ulevi, usharati na kazalika. Utawasikia wakisema eti: "Baba fulani akitenda hivi na mimi napashwa kumuonyesha kama nipo mwanamke."

Mme anaposhikwa na hasira ndipo wanafikia vita na fujo nyumbani.

Wengine hufanya kusudi na kufika nyumbani usiku kati nyuma ya bwana zao.

Tupo hakika kuwa unyumba siyo gereza. Kitu cha lazima ni masikilizano na kutambuana tabia kati ya mke na mme. Bila kusahau kuvumiliana. Tukifanya hivyo mambo mengi yatatendeka sawa. Kwani yafaa kujua ya kama vyote tufanyavyo ni kwa ajili ya watoto wetu.

Pahali pengine,utawaona wa bibi wengine wenyi "waliweza kujinyakulia ushindi nyumbani mwao" kuwapatisha mabwana zao haya mbele ya watu wakisema :"Eti aka ndio kabwana gani ?"

Kisha ugonvi kidogi tu huwasikia wenyi kusema :"Sawa tu. Nyumba hii tutaiacha. Kila mtu atarudi kwao. Hata watoto hawa." Zaidi tusishangae kuona mabwana wengi wenyi kutupwa nje na bibi zao eti : "Nyumba hii ni mimi ndiye niliinunua, kwanza ka weye haunistahili..."

Wabibi wapenzi, mambo hayo ni sawa ? Huo ni ungwana ?

Barhayiga Shafari


# JUA

## Gazeti la Kivu


KABOYI HABIMANA.-

# Mabadiliko muhimu katika uongozi wa vikundi vya askari jeshi

Kufuatana na hatua N° 254 na 255, mareshali Mobutu Sese Seko anatoka kuwataja viongozi wapya wa majimbo pamoja na makamu wao.

Wawili miongoni mwa maliwali hao walibaki nafasi zao za zamani. Ni pamoja Mwando Nsimba (Kivu) na Makolo Jibikilay (Zaïre ya Chini). Daftari ya majina ya maliwali na makammu wao ilipangwa namna ifuatayo :

-Bandundu :
 .Sambia Geredanu
 .Dibenga Tshibudi
-Zaire ya Chini :
 .Makolo Jibikilay
 .Djoho Tayeta
-Ekwatori :
 .Mpambia Musanga Bekaja
 .Mokolo Matamba
-Zaire ya Juu :
 .Salumu Amisi
 .Mujinga N'Swana Samukasa



-Kasai ya Magharibi
 .Bangala Basila
 .Mwenelwata Isungampala
-Kasai ya Mashariki
 .Konde Vila Kikanda
 .Koya Dialo
-Kinshasa :
 .Tshimbombo Mukuna
 .Nzita Puati
 .Nkoy Mafuta (mwanamke)
-Kivu :
 .Mwando Nsimba
 .Endjonga Bokwa
-Shaba :
 .Duga Kugbe Toro
 .Sabi Mobyem

Katika harakati zake za ujenzi wa nchi, askari jeshi wetu hawakubaki nyuma. Ni hivi jemadari Singa Boyende alichaguliwa na mareshali Mobutu kama vile mchunguzi mkuu wa askari jeshi. Wananchi Etampo, Babia Bumba, Danga, na Ebayo waliamriwa waingie katika mapumziko.

Jimbo la kwanza la askari (Shaba na Kasai) litaongozwa na Koloneli Mayele, jimbo la pili (Kinshasa, Bandundu na Zaire ya chini) litakuwa chini ya uchunguzi wa koloneli Bakambala na lile la tatu (Zaire ya juu) na Koloneli Shabani.

Maafisa ambao majina yao yaandikwa hapa chini ndio wataongoza matawi ya askari jeshi:

1) Pambu Kinkela,
2) Engwongwo Moze,
3) Kapesa Dunia,
4) Muleji kaula,
5) Ngomba Engia Sa,
6) Makuta Esapia,
7) Akeye Ansoni,
8) Tshikudi Bakajika.

### JE UMESIKIA ...?

**KWAMBA** shirika linalohusika na ugawaji wa nguvu za umeme kwa kifupi cha kifaransa SNEL latutia lisani pembeni ?
Siku hizi wakaaji wa mitaa ya Kadutu na Bagira wabaki katika giza usiku ingawa kila mara waazimishwa kulipa gharama nyingi.
Majambazi wapo katika furaha kubwa kwani wafanya kazi yao bila tatizo lolote. Kwa mfano kuwakunguta raia usiku na kuwanyanganya mali zao hata kufikia vifaa kama vile feza,nguo na hata viatu.
Wajificha katika giza. Wanaposhambulia mtu fulani na wakati huyo anapolalamika,wakaaji huogopa kuamka kwani hawana namna ya kuona yale yanayopita nje.

**KUWA** viongozi wa mikoa ya Bukavu hawashurulike na afya ya raia ?
Wakaaji hupiga kelele ya yohe kutokana na magonjwa mbali mbali yanaowashambulia. Miongoni mwa magonjwa hayo,twaweza kutaja ule wa kipindupindu tunaozoea kuita cholera.
Bila kusahau kuhara na vivi hivi.
Viongozi wa mikoa waomba kila mara watu wafanye kazi za "salongo" wakisahau kuwapatia raia mashauri muhimu kuhusu kanuni za afya na kuwahimiza wafanye vyote wawezavyo kwa kuepuka magonjwa.
Kazi yao ni kuwafuata waakaji wanaokutaniwa katika kosa fulani kusudi wawapatie "lwa sombe".

# Vita kali kwa kupinga kipindupindu

Katika toleo letu n° 642, tuli wafasiria wasomaji wetu machache kuhusu namna ya kupinga ugonjwa wa kipindupindu unaojulikana hasa hapa mjini Bukavu kwa jina la Choléra.

Alipofika hapa mjini Bukavu akitokea Lubumbashi kupitia Kinshasa, mganga mchunguzi wa jimbo la Kivu, mwananchi Ngoma alieleza kuwa alitumwa haraka haraka na liwali wa jimbo mwenyewe, mwananchi Mwando kusudi afanye vyote awezavyo kwa kupiganisha cholera.
Mwananchi Ngoma alinena kuwa cholera ina viini vyake. Ni pamoja na kuhara bila kiasi na kutapika ovyo. Yule anayeshikwa na kipindupindu anaendesha mavi inayosura ya maji ya mchele. Ugonjwa huo mkali uliingia katika jimbo la Kivu ukitoka katika jamhuri jirani Tanzania kwa njia ya maji.

Kwa kupinga visa vya ugonjwa huo, vituo vitatu vya afya vimeshimikwa Kadutu, Nguba na kunako hospitali kuu ya mji wa Bukavu. Ni hivi inaombwa kwa watu wote kuwapeleka wagonjwa wa cholera katika vituo hivyo vya afya bila kusita. Lakini mbele ya yote, yafaa kumtolea mgonjwa maji ambamo muna nusu ya sukari pamoja na chumvi.
Watu wote waombwa kuchemsha maji mbele ya kuyanywa kwani hata yale maji ya REGIDESO yana pia uchafu ndani yake.
Wakaaji wakatazwa kula vyakula vibichi vinavyouzishwa ovyo ovyo sokoni. Yule anayeshikwa na ugonjwa wa kipindupindu hawezi kufinikwa wakati wa usiku.
Wasafiri waombwa kuchanjwa ma dawa ya kujikinga kwa cholera mbele ya kutoka Kivu na kujielekeza mahali pengine.

*Imegeuzwa na Kaboyi Habimana*

BUMBUAZI

### FUNGUENI MACHO !

Majambazi wanaotumia bunduki, gongo na mipanga watetemesha siku hizi wakaaji wa mji wa Bukavu.
Kila mara wakati watenda maovu hao wanapojinyakulia mali ya raia, watafutwa nafasi zote na walinda amani ila hawaonekane.
Unaposhambuliwa wakati wa usiku, hata ukipiga kelele ya yowe hakuna jirani anayepata uhodari wa kuamka kwa kukusaidia. Majirani wajifungia nyumbani kwao kwani yule anayesubutu kutoka nje aweza akajionee "cha mtema kuni".

Raia wahitaji walindwe vizuri pamoja na mali zao.
Wale wanaohusika wachungue vema jambo hilo.